



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU

01/01/2025

TANGAZO KWA UMMA

KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 8 (1)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Kasulu anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vyenye sifa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya shilingi **500,000,000** zimetengwa katika robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika ofisi ya serikali za vijiji iliyopo katika kata.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri,
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasirimali,
- (iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6 (1) (d) mtu mwenye ulemavu unaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine,
- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wenye namba za Nida na wasio na ajira rasmi (wasiwe waajiriwa wa serikali), wenye akili timamu na wenye umri

- (vi) wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kiwe na wanakikundi wenyе umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na afisa maendeleo ya jamii wa kata husika au mtendaji wa kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo;

1. Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na afisa mtendaji wa kijiji
2. Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo
3. Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyondani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki
4. Kwa Vikundi vinavyoomba vyombo vyaya usafiri waambatishe leseni pamoja na cheti cha mafunzo ya udereva.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 31/01/2025 saa 9:30 alasiri

Tangazo hili limetolewa na: -



.....

Dkt Semistatus H.Mashimba

MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA

KASULU

